East African Journal of Swahili Studies
eajss.eanso.org
Volume 7, Issue 1, 2024
Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

Original Article

Maana za Majina ya Asili ya Watoto katika Jamii ya Waasu

Janeth Jafet[1] *na Perida Mgecha, PhD*[2*]

[1] Shule ya Sekondari Kitefu, S. L. P. 15258, Njiro-Arusha, Tanzania.
[2] Chuo Kikuu Tumaini Makumira, S. L. P. 55, Usa River, Arusha, Tanzania.
[*] ORCID ID: https://orcid.org/0009-0009-6177-8282; Barua pepe ya mawasiliano: peridamgecha@gmail.com

DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1826

Tarehe ya Uchapishaji:

15 Machi 2024

Istilahi Muhimu:

Maana, Majina, Kichasu, Jamii ya Waasu.

IKISIRI

Makala hii inachunguza maana za majina ya asili ya watoto katika jamii ya Waasu. Malengo mahususi yakiwa kwanza kubaini majina ya asili ya watoto, na pili kueleza maana zilizobebwa na majina hayo. Utafiti huu ni wa kitaamuli hivyo umetumia usanifu wa kifenomenolojia. Watoataarifa waliohusika katika kutoa data ni 18 ambao wamepatikana kwa mbinu ya usampulishaji tabakishi na usampulishaji tajwa. Data za makala hii zimekusanywa kwa kutumia mbinu ya usaili na majadiliano ya vikundi lengwa; kisha zikachanganuliwa kwa mbinu ya kusimba maudhui. Nadharia ya Uumbaji iliyoasisiwa na Sapir (1958) ndiyo iliyotumika katika makala hii. Matokeo yamebainisha majina ya asili ya watoto 145. Maana za majina haya zimegawanyika katika makundi yafuatayo: majina yenye maana zitokanazo na imani kwa Mwenyezi Mungu, mahali mtoto alipozaliwa, wanyama, misimu ya miaka na siku, majanga, vyakula na matukio ya furaha. Utafiti huu una mchango mkubwa katika kuhifadhi historia, na utamaduni uliojificha katika lugha ya Kichasu. Hata hivyo, tafiti zaidi kuhusu majina zifanyike katika jamii nyingine kwani jamii zinatofautiana katika asili, historia, shughuli za kijamii na utamaduni.

APA CITATION

Jafet, J. & Mgecha, P. (2024). Maana za Majina ya Asili ya Watoto katika Jamii ya Waasu. *East African Journal of Swahili Studies*, *7*(1), 170-181. https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1826.

CHICAGO CITATION

Jafet, Janeth and Perida Mgecha. 2024. "Maana za Majina ya Asili ya Watoto katika Jamii ya Waasu". *East African Journal of Swahili Studies* 7 (1), 170-181. https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1826.

HARVARD CITATION

Jafet, J. & Mgecha, P. (2024) "Maana za Majina ya Asili ya Watoto katika Jamii ya Waasu", *East African Journal of Swahili Studies*, 7(1), pp. 170-181. doi: 10.37284/jammk.7.1.1826.

IEEE CITATION

J. Jafet & P. Mgecha "Maana za Majina ya Asili ya Watoto katika Jamii ya Waasu", *EAJSS*, vol. 7, no. 1, pp. 170-181, Mar. 2024.

MLA CITATION

Jafet, Janeth & Perida Mgecha. "Maana za Majina ya Asili ya Watoto katika Jamii ya Waasu". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 7, no. 1, Mar. 2024, pp. 170-181, doi:10.37284/jammk.7.1.1826.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1826

UTANGULIZI

Majina ya asili ni majina ambayo chimbuko, historia, na maana yake hutokana na vigezo, taratibu na kanuni zilizobeba maana kulingana na mila, desturi, na utamaduni wa jamii husika. Majina hayo hutolewa katika familia baada ya mtoto kuzaliwa. Mara nyingi hutolewa na watu maalum kama vile bibi, babu au shangazi. Hata hivyo suala la utoaji majina kwa watoto hutofautiana kati ya jamii na jamii au ukoo na ukoo. Utoaji wa majina ya asili kwa mtoto ni tukio muhimu sana katika jamii za Kiafrika (Muzale, 1998). Kamusi Kuu ya Kiswahili (2015) wanadai kuwa jina ni neno linalotumika kutaja mtu au kitu. Hivyo majina ni maneno yanayotaja vitu, viumbe, au hali ili kuviainisha au kuvitofautisha na vitu vingine. Massamba (2009) anabainisha aina za majina kama vile majina ya familia, majina ya koo na majina ya vitu na mahali. Anaongeza kuwa majina haya huwa ni utambulisho wa jamii. Aidha Kihore (2009) anabainisha aina tatu za majina ambazo ni majina jumuishi, majina ya pekee na majina ya kundi. Makala hii imejikita katika majina ya asili katika familia, wanayopewa watoto ambayo huhusisha kikundi cha watu.

Kama ilivyo katika maneno mengine katika lugha kwamba lazima yabebe maana kulingana na muktadha wake ndivyo ilivyo kwa majina kwamba lazima yawe na maana fulani kulingana na muktadha ambamo lugha hiyo inatumika. Massamba (2009) anafafanua maana kuwa ni kile ambacho neno huashiria kutokana na ama dhana, matumizi au kitajwa. Resani (2017) anaeleza kuwa maana ya maana ni tafsiri anayokuwa nayo msemaji au msikilizaji na kwamba maana huwezi kuiona bali huwa katika ubongo wa mtu anayeitafsiri. Kwa ujumla maelezo yaliyotolewa na wataalamu hapo juu yanaonyesha kuwa maana inatokana na ama dhana ya kitu kilichotajwa au matumizi yake, na maana hiyo huwa katika ubongo wa mtumiaji wa lugha husika. Hivyo makala hii inachunguza maana za majina ya asili ya watoto katika jamii ya Waasu wanaoishi mkoa wa Kilimanjaro hasa katika wilaya ya Same. Malengo mahususi ya makala hii ni mawili: kwanza, ni kubainisha majina ya asili wanayopewa watoto wa jamii ya Waasu; pili ni kuchambua maana za majina hayo.

MAPITIO YA MAANDIKO

Suala la utoaji wa majina kwa watu au vitu ni mada ambayo imeshughulikiwa na baadhi ya watafiti wa lugha. Agyekum (2006) amefanya utafiti kuhusu majina ya watu wa kabila la Akan nchini Ghana; akagundua kuwa watu wa kabila la Akani huwapa watoto majina kulingana na siku za kuzaliwa, familia aliyozaliwa, tukio la tohara, athari za kimaumbile, kama watoto wamezaliwa pacha, dini, majina ya kimuujiza, majina yanayotokana na mafanikio majina ya vijembe na methali, majina ya umbo la mwili wa mtoto aliyezaliwa na majina ya ukoo. Utafiti huu umekuwa na mchango katika makala hii kwani umeonyesha maana na mazingira yanayopelekea watoto kupewa majina ya asili katika jamii. Hata hivyo makala hii imejikita kuchunguza majina wanayopewa watoto katika jamii ya Wachasu.

Aidha Baitani (2010) akizungumzia majina ya watu wa kabila la Wahaya anasema kuwa majina ya Kihaya yanatokana na matukio fulani, itikadi na jinsi. Mfano mtoto aliyezaliwa baada ya mapacha, mtoto aliyezaliwa baada ya baba yake kufa akiwa bado yuko tumboni mwa mama yake kwa kawaida Wahaya huwapa majina tofauti. Mfano *Ishengoma*, mapacha wa kiume aliyetangulia kuzaliwa, wa kike huitwa Nyangoma, wanaofuata wakiwa mapacha mwanaume huitwa *Kato* na mwanamke huitwa *Nyakato*. Hata kama utafiti huu unaongeza maarifa katika kuchunguza maana za majina bado makala hii ni muhimu kwani inachunguza maana za majina ya asili ya watoto katika jamii ya Waasu ambayo ni tofauti na ile jamii iliyochunguzwa na Baitan. Pia kila jamii ina utaratibu wake na utamaduni wake katika utoaji wa majina.

Azael (2013) amechunguza matumizi ya majina ya asili katika jamii ya Kiuru. Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kwamba majina katika jamii ya Wauru hutolewa kwa kuzingatia namna mtoto alivyozaliwa na baada ya kujifungua. Utafiti huu pia umebainisha kuwa majina ya Kiuru yanatokana na mambo mbalimbali kama vile tabia

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1826

ya mtoto, maumbile/mwonekano wa mtoto pindi alipozaliwa au wakati wa malezi, matukio mbalimbali ya kijamii, vipindi mbalimbali katika jamii na misingi ya imani na desturi za Wauru. Utafiti wa Azael (keshatajwa) umesaidia kujua asili ya majina wanayopewa watoto katika jamii ya Waasu. Aidha Nyanganywa (2013) na Lenjima (2019) wote wamechunguza majina ya watu katika jamii ya Wajita nchini Tanzania. Nyanganywa (keshatajwa) utafiti wake umejikita kuchunguza semantiki ya majina na taratibu za utoaji wa majina hayo katika jamii ya Wajita. Matokeo yamebaini kuwa majina ya Kijita hutolewa kwa kuzingatia utaratibu fulani unaojikita katika falsafa, mila na desturi za Kijita. Utafiti wa Nyanganywa umejikita zaidi katika semantiki ya majina wakati makala hii imezingatia maana ya kisemantiki na ya kipragmatiki. Aidha utafiti wa Lenjima (keshatajwa) katika lugha ya Kijita umejikita kuchunguza maana, mambo yanayopelekea watu kupewa majina ya asili na faida ya kuwapa watu majina ya asili. Tofauti na makala hii, utafiti wa Lenjima umemakinikia majina katika jamii ya Wajita na umechunnguza majina kwa ujumla wakati makala hii imejikita katika jamii ya Wachasu kwa kumakinikia maana za majina wanayopewa watoto.

Resani (2016) pia ametafiti maana ya majina katika jamii ya Wabena akijikita zaidi katika vigezo vinavyotumika kuwapatia watoto majina. Anafafanua kuwa katika jamii ya Wabena wazazi huwarithisha watoto majina ya watu waliokuwa na wasifu mzuri kama vile wakulima hodari, wawindaji, wahunzi, matajiri wakubwa na watawala wa jadi (machifu). Utafiti huu umedhihirisha kuwa watoto au watu wazima hupewa majina yanayokosoa tabia zisizotakiwa katika jamii na wengine hupewa majina yanayoashiria kumaliza matatizo yaliyofululiza kutokea katika ukoo au familia. Mfano, *Tumwanukye* maana yake tumempokea, jina hili hupewa mtoto aliyezaliwa nje ya ndoa, *Lunyodzi* na *Dzivembela* yakimaanisha lilia, haya ni majina ya watoto wanaozaliwa baada ya majonzi katika familia. Hata kama utafiti huu umesaidia kuthibitisha kuwa majina hutolewa kwa sababu fulani, hata hivyo tunaona umejikita katika jamii ya Wabena na umeangalia majina kwa ujumla wakati makala hii inachunguza maana ya majina ya watoto katika jamii ya Waasu.

Halikadhalika, Nyiti (2021) ametafiti maana ya majina ya koo katika jamii ya Wameru. Katika utafiti wake amechunguza maana ya majina ya koo na sababu za kutoa majina ya koo katika jamii ya Wameru. Matokea ya utafiti huu yameonyesha kuwa majina ya koo yana maana kutokana na utamaduni wa Wameru. Mfano ukoo wa *Ayo* maana yake ni huyo, *Mbise* maana yake mfiche, *Nyiti* maana yake ni kukataa au kugoma, *Mafie* maana yake ni nyani. Pia ameeleza sababu za kutoa majina ya koo katika jamii ya Wameru ambazo ni tabia ya mtu, kufanya kazi kwa bidii na majina ya koo yaliyosababishwa na sifa za wanyama. Utafiti huu umewaongezea maarifa watafiti katika kuchunguza majina ya asili ya watoto ambayo yamebeba maana kutokana na utamaduni wa jamii ya Waasu. Hata hivyo utafiti wa Nyiti (keshatajwa) umejikita kwenye maana za majina ya koo katika jamii ya Wameru wakati makala hii inachunguza maana za majina ya watoto katika jamii ya Wachasu. Aidha Elihaki (2012) ametafiti majina ya mahali katika jamii ya Waasu. Lengo mojawapo la utafiti wake likiwa kuchunguza maana ya majina ya mahali katika jamii ya Wachasu. Matokeo ya utafiti huo yamedhihirisha kuwa majina ya mahali yana maana zitokanazo na majina ya watu, koo za watu, wanyama, miti/mimea na maana zingine zinatokana na matukio mbalimbali. Utafiti wa Elihaki unatofautiana na makala hii kwani inachunguza maana za majina ya asili ya watu na siyo mahali ikijikita zaidi katika majina ya asili ya watoto katika jamii ya Waasu.

Ingawa kipengele cha majina kinaonekana kushughulikiwa na wanaisimu wengi kama waliotajwa hapo juu, tafiti hizo tangulizi zimemakinikia zaidi katika kuchunguza majina ya watu kwa ujumla, majina ya koo na majina ya mahali. Pamoja na hayo tafiti hizo nyingi zimefanyika katika lugha nyingine na siyo Kichasu, isipokuwa Elihaki (2012) ambaye alifanya kwenye Kichasu kwa kuchunguza majina

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1826

ya mahali. Makala hii imemakinikia kuchunguza maana za majina ya asili ya watoto katika jamii ya Waasu. Watafiti wameamua kumakinikia majina ya asili ya watoto badala ya majina ya watu wazima kwa sababu utamaduni wa jamii yoyote ile upo katika majina na pindi mtoto anapozaliwa na kupewa jina la asili hutunza utamaduni wa jamii yake. Wakati mtoto anapokua na kuwa mtu mzima huweza kubadili jina la utotoni na kuwa na jina lingine ambalo sio la asili ya jamii yake. Mambo yanayoweza kumfanya mtu kubadili jina la asili alilopewa utotoni inaweza kuwa dini ambapo mtu anaweza kubatizwa na kubadili jina; maendeleo ya elimu pia huweza kumfanya mtu kubadili jina la utotoni. Hivyo utafiti huu hasa umemakinikia kubainisha majina ya asili ya watoto na kuchambua maana za majina hayo.

Kiunzi cha Nadharia

Makala hii inaongozwa na nadharia ya Uumbaji iliyoasisiwa na Sapir (1958) na kuendelezwa na mwanafunzi wake Benjamini Lee Whorf mwaka huo huo wa 1958. Nadharia hii inahusu lugha na utamaduni wa jamii. Sapir aliamini kuwa upo uhusiano wa lugha na jamii hivyo lugha hutawala fikra za wazungumzaji wake na kuwapa namna ya kusawiri ulimwengu wao. Sapir anaendelea kusema kuwa lugha ndio msingi wa kuuelewa ulimwengu. Unapojifunza lugha ni kama unatawaliwa na lugha hiyo hata dunia utakayoiumba akilini mwako itatokana na dunia kama ilivyoratibiwa na wasemaji wake. Binadamu huona ulimwengu kupitia taratibu zilizowekwa na lugha yake ya kwanza. Ni vigumu kuchukua jina la mtu kutoka katika jamii fulani na kumpa mtu wa jamii lugha nyingine kwa sababu jina la jamii moja hufungamana na imani hiyo ambayo huambatana na utamaduni wa jamii husika.

Nadharia ya Uumbaji imejengwa katika mihimili ifuatayo:

- Lugha ndio msingi wa kuuelewa ulimwengu.
- Fikra za mtu yeyote huamliwa na lugha anayoizungumza.
- Lugha huathiri namna watu wanavyoumba ulimwengu wao.
- Watu wanaozungumza lugha fulani huuona na kuufasili ulimwengu tofauti na wanaozungumza lugha nyingine.
- Hakuna jamiilugha mbili zinazoweza kuwa sawa hivyo hata maana za majina katika jamii mbalimbali haziwezi kuwa sawa.

Nadharia hii imekuwa faafu katika makala hii kwani inaonyesha kuwa fikra za wanajamii huamliwa na lugha wanayotumia. Aidha majina yao hutokana na lugha na fikra zao hivyo nadharia hii imewasaidia watafiti kubaini majina ya asili ya watoto pamoja na maana zake katika jamii ya Waasu kwani lugha ya Kichasu ndiyo inayoamua ulimwengu au mazingira ya Waasu katika utoaji wa majina ya watoto.

METHODOLOJIA YA UTAFITI

Sehemu hii inahusu mbinu mbalimbali zilizotumiwa na watafiti katika kufanikisha kazi hii. Mbinu hizo ni pamoja na mkabala wa utafiti, usanifu wa utafiti, eneo la utafiti, wango, usampulishaji, sampuli, mbinu za ukusanyaji data na uchanganuzi wa data.

Mkabala, Usanifu wa Utafiti na Usamplishaji

Utafiti huu uliongozwa na mkabala wa kitamuli. Mkabala wa kitaamuli hutumia mbinu za kimaelezo na kifafanuzi katika kutafuta maarifa ya kutatua tatizo fulani au kuongeza maarifa (Creswell & Creswell, 2022). Mkabala huu uliwawezesha watafiti kupata maelezo ya kina kuhusu majina ya asili ya watoto na maana zake katika jamii ya Waasu. Kadhalika mkabala huu uliwawezesha watafiti kuchanganua data na kuandika ripoti iliyofafanua vyema maana za majina ya asili ya watoto katika jamii ya Waasu.

Katika kuchunguza maana za majina ya asili ya watoto katika jamii ya Waasu, watafiti waliamua kutumia usanifu wa kifenomenolojia kwani unachambua tabia, tukio au dhana, uzoefu au jambo halisi na mahususi ambalo kuwapo kwake kunadhihirika (Ponera, 2019). Katika utafiti huu

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1826

fenomena ni maana za majina. Aidha katika kuchunguza fenomena hiyo watafiti walibaini majina ya asili ya watoto na maana zake katika jamii ya Waasu, ambalo ni jambo linajulikana na kudhihirika katika jamii hiyo. Utafiti ulifanyika katika mkoa wa Kilimanjaro wilaya ya Same ambapo wapo Waasu wanaozungumza lugha ya Kichasu.

Katika utafiti huu mbinu za usampulishaji tabakishi na usamplishaji tajwa zilitumika katika kuwapata watoataarifa. Usampulishaji tabakishi ulitumika kuwapata Waasu walio kwenye tabaka la umri wa miaka 23-54 ambao walikuwa 12 wakati usampulishaji tajwa ulitumika kuwapata Waasu wenye umri wa miaka 55 na kuendelea ambao walikuwa 6. Jumla ya watoataarifa walikuwa 18 ambao walipatikana kutoka katika kata tatu Bwambo, Kirangare na Vunta kama *Jedwali 1* linavyoonesha.

Jedwali 1: Sampuli ya Watoataarifa

Kata	Umri	Idadi ya Watoataarifa	Jumla
Bwambo	23-54	4	6
	55 na kuendelea	2	
Kirangare	23-54	4	6
	55 na kuendelea	2	
Vunta	23-54	4	6
	55 na kuendelea	2	
Jumla		18	18

Watafiti walitumia watoataarifa wenye umri wa miaka 23-54 kwa sababu wengi wao wapo katika umri wa kuzaa watoto na hivyo wana mchango katika utoaji wa majina ya asili kwa watoto, na pia walitumia watoataarifa wa umri wa miaka 55 na kuendelea kwani ni watu wazima na wana ujuzi mwingi wa majina ya asili katika jamii ya Waasu.

Mbinu za Ukusanyaji na Uchanganuzi wa Data

Mbinu za kukusanyia data zilikuwa ni usaili na majadiliano ya vikundi lengwa ambapo zote zilitumika katika kupata data za malengo husika ambayo ni kubainisha majina ya asili ya watoto na maana zake. Mbinu ya usaili ilitumika kwa watoataarifa wenye umri wa miaka 55 na kuendelea ambao walikuwa 6. Watoataarifa hawa walibaini majina mia moja na maana zake. Mbinu ya majadiliano ya vikundi lengwa ilitumika kwa watoataarifa wenye umri wa miaka 23-54 ambapo walibaini majina 45 na maana zake. Data za utafiti huu zilichanganuliwa kwa mbinu ya kusimbisha maudhui. Hata hivyo, katika mchakato wa ukusanyaji wa data, watoataarifa walipewa uhuru wa kuamua kushirika au kutokushiriki, kurekodiwa au kutokurekodiwa. Hivyo walioshiriki katika utafiti huu ni wale tu waliokubali kwa ridhaa yao wenyewe.

MATOKEO YA UTAFITI

Makala hii imelenga kuchunguza maana za majina ya asili ya watoto katika jamii ya Waasu. Data zimewasilishwa na kuchambuliwa kulingana na malengo mahususi ambayo ni kubainisha majina ya asili ya watoto na maana za majina hayo katika jamii ya Waasu.

Majina ya Asili ya Watoto katika Jamii ya Waasu

Lengo la kwanza la utafiti ni kubainisha majina ya asili ya watoto katika jamii ya Waasu. Data za lengo hili zimekusanywa kwa mbinu ya usaili na majadiliano ya vikundi lengwa ambapo watafiti wamebaini jumla ya majina 145 ya asili wanayopewa watoto katika jamii ya Waasu. Yafuatayo katika *Jedwali 2* ni baadhi ya majina ya asili ya watoto katika jamii ya Waasu kama yalivyobainishwa na watoataarifu wenye umri wa miaka 23-54.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1826

Jedwali 2: Majina ya asili ya watoto katika jamii ya Waasu kama Yalivyobainishwa na watoataarifa wenye umri wa miaka 23 -54

Jina	Jinsi	Jina	Jinsi	Jina	Jinsi
Gwirisha	Me	Namwai	Ke	Nikombolwe	Me
Lukio	Me	Nangasu	Ke	Nimzihirwa	Me
Mshighwa	Ke	Narindwa	Ke	Niomba	Me
Nabera	Ke	Nasemba	Ke	Nirindiwe	Ke
Nafwiwa	Ke	Nasembiwa	Ke	Sekani	Me
Nagenjwa	Ke	Nasikiwa	Ke	Taseni	Me
Nainkwa	Ke	Navoneiwa	Ke	Tuzihirwe	Me
Nakijwa	Ke	Nazahedi	Ke	Twamzihirwa	Me
Nakombolwa	Ke	Nazihirwa	Ke	Twazihirwa	Me
Namseka	Ke	Ngasu	Me	Zihirwani	Me

Majina ya asili ya watoto katika jamii ya Waasu yapo mengi kwani watoto huzaliwa kila siku na hupewa majina kila siku. Katika *Jedwali 2* yapo majina ambayo huweza kupewa watoto wa kike na wa kiume mfano jina *Ngasu*. Pia yapo majina ambayo hayafanani kwa wanaume na wanawake majina hayo kwa takwimu ndio mengi katika jamii ya Waasu mfano *Lukio* linatumika kwa wanaume tu na *Nagenjwa* linatumika kwa wanawake tu.

Hata hivyo, katika makala hii majina mengi ya asili ya watoto yamebainishwa na watu wenye umri mkubwa ambao ni miaka 55 na kuendelea. Baadhi ya majina hayo yamebainishwa katika *Jedwali 3*.

Jedwali 3: Majina yaliyotajwa na watu wenye umri wa miaka 55 na kuendelea

Jina	Jinsi	Jina	Jinsi	Jina	Jinsi
Berya	Me	Nakiete	Ke	Nisagurwe	Me
Elijenja	Me	Nakio	Ke	Nisembiwa	Me
Elisamehe	Me	Namkuyu	Me	Ntegenjwa	Ke
Elitogola	Me	Namtaso	Me	Rindeni	Me
Izungo	Me	Namweta	Me	Sekiete	Me
Kianda	Me	Namweta	Me	Semgonja	Me
Kisaka	Me	Nanzano	Ke	Semshitu	Me
Mbonea	Me	Nanzia	Ke	Sengasu	Me
Mjeni	Me	Nasembiwa	Ke	Senzia	Me
Mweta	Me	Nasharu	Ke	Togolani	Me
Naelijwa	Ke	Natogola	Ke		
Nagwira	Ke	Niarira	Me		

Jedwali 3 linawasilisha majina 34 tu kati ya majina 115 yaliyobainishwa na watoataatifa wenye umri wa miaka 50 na kuendelea. Hivyo makala hii imebainisha jumla ya majina 145, majina 30 yakiwa yamebainishwa na watoataarifa wenye umri wa miaka 23-54 na majina 115 yakibainishwa na watoataarifa wenye umri wa miaka 55 na kuendelea. Hivyo, watu wenye umri mkubwa walionekana kuwa na ujuzi wa kuyajua vizuri majina mengi ya asili ya watoto wa jamii ya Waasu.

Maana ya Majina ya Asili ya Watoto katika Jamii ya Waasu

Hili ni lengo la pili la makala hii ambalo limelenga kujua maana zilizobebwa na majina ya asili ya watoto katika jamii ya Waasu. Makala hii imebaini kuwa yapo majina ya asili ya watoto yenye maana zitokanazo na imani kwa Mwenyezi Mungu, mahali, wanyama, misimu ya miaka na siku, majanga, vyakula na matukio ya furaha. Maana hizo zimefafanuliwa kama ifuatavyo.

Majina ya Watoto ya Asili Yenye Maana Itokanayo na Imani

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1826

Makala imeonyesha kuwa yapo majina ya asili ya watoto katika jamii ya Waasu yatolewayo kutokana na imani aliyokuwa nayo mtu kwa Mungu wake au kile kitu binadamu anachokiabudu. Katika *Jedwali 4* majina hayo yamefafanuliwa.

Jedwali 4: Majina ya asili ya watoto yenye maana itokanayo na imani

Jina	Jinsi	Maana	Jina	Jinsi	Maana
Elijenja	Me	Mungu saidia	Nasembiwa	Ke	Nimeombewa
Elitogola	Me	Msifu Mungu	Namsemba	Ke	Namwomba
Gwirisha	Me	Shika sana	Nasikiwa	Ke	Nimesikilizwa
Lukio	Me	Uponyaji	Navoneiwa	Ke	Nimefadhiliwa
Mbonea	Me	Neema	Niarira	Me	Naamini
Naelijwa	Ke	Nimetakaswa	Nikombolwe	Me	Nimekombolewa
Nagwira	Ke	Nimepokea	Nirindiwe	Ke	Nimesubiriwa.
Nainkwa	Ke	Nimepewa.	Nisagurwe	Me	Nimechaguliwa
Nakijwa	Ke	Nimeponywa	Nisembiwa	Me	Nina bembelezewa
Nakombolwa	Ke	Nimekombolewa	Ntegenjwa	Ke	Nilisaidiwa
Namtaso	Me	Mtu wa maombi	Rindeni	Me	Ngojeni
Narindwa	Ke	Nimelindwa na Mwenyezi Mungu	Taseni	Me	Ombeni
Nasemba	Ke	Kuomba kwa kubembeleza	Togolani	Me	Sifuni

Katika jamii ya Waasu dini ya Kikristo imetawala zaidi ya dini zingine hivyo hali hii hufanya watoto wapewe majina ya asili yanayotokana na imani hiyo zaidi.

Majina ya Asili ya Watoto Yenye Maana Itokanayo na Mahali Mtoto Alipozaliwa

Katika jamii ya Waasu majina yanatolewa kutokana na eneo au mazingira mtoto alipozaliwa. Data zilizokusanywa zimedhihirisha hilo kama ilivyofafanuliwa katika *Jedwali 5*.

Jedwali 5: Majina ya watoto yenye maana itokanayo na mazingira mtoto alipozaliwa

Jina	Jinsi	Maana	Jina	Jinsi	Maana
Izungo	Me	msitu mdogo.	Namweta	Me	Jito
Kianda	Me	Mto	Namweta	Me	Wa mtoni
Kisaka	Me	Kichaka	Nanzia	Ke	Wa njiani
Mjeni	Me	Mgeni	Sekaya	Me	Wanyumbani
Mweta	Me	Jito	Sekiete	Me	Wa sokoni
Nakaya	Ke	Wa nyumbani	Semgonja	Me	Wa Gonja
Nakiete	Ke	Wa sokoni	Sempombe	Me	Wa maji
Nakisaka	Ke	Wa kichakani	Semshitu	Me	Wa msituni
Namkuyu	Me	wa mkuyu	Sengasu	Me	unyago
Nampombe	Ke	Maji	Senzia	Me	Wa njiani

Watu wa jamii ya Waasu hupenda kuwapatia watoto wao majina kulingana na eneo mtoto alipozaliwa. Wanaamini kuwa eneo mtoto anapozaliwa lina maana katika maendeleo ya ukuaji wa mtoto na hata atakapokuwa mtu mzima huwa na sifa za eneo alilozaliwa mfano, jina *Mweta* linamaanisha mto mkubwa hivyo mtoto huyo akikua huwa na nguvu kama mto mkubwa.

Majina ya Asili ya Watoto yenye Maana Itokanayo na Wanyama

Katika jamii ya Waasu baadhi ya majina ya asili ya watoto yamebeba maana itokanayo na wanyama. Utafiti umeonyesha kuwa majina hayo yana maana ya wanyama wa kufugwa au wa porini. Watoataarifa 12 wameonyesha kwa kutaja baadhi ya wanyama hao kwa mfano tembo, nyani, paka na nyoka. Katika *Jedwali 6* majina hayo yamefafanuliwa.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1826

Jedwali 6: Majina ya Asili ya Watoto yenye Maana Inayotokana na Wanyama

Jina	Jinsi	Maana	Jina	Jinsi	Maana
Fue	Me	Nyani	Nankebe	Ke	Tumbili
Kachua	Me	Chura	Nantembo	Ke	Tembo
Koboro	Me	Kobe	Nyaki	Me	Nyani
Mathogi	Me	Punda	Seng'onji	Me	Kondoo
Nachua	Ke	Tembo	Senkebe	Me	Tumbili
Naigonji	Ke	Kondoo	Sentembo	Me	Tembo
Nambuji	Ke	Mbuzi	Senyari	Me	Nyani

Matokeo yanaonyesha kuwa watoto wanapewa majina ya asili yenye maana ya wanyama kwani wanyama hao wanapatikana katika maeneo ya jamii hii, na pia wanyama kama ng'ombe, kondoo, mbuzi wanafugwa na kutunzwa katika familia za Waasu. Waasu hupenda kuwapa watoto baadhi ya majina hayo kutokana na tabia za wanyama hao. Mfano jina *Fue* maana yake ni nyani, hii ina maana mtoto anafanana na nyani au ana tabia za udokozi kama nyani. *Sentembo* ni mtoto mwenye mwili mkubwa na *Naigonji* mtoto mjingamjinga, *Nankebe* ni mtoto mwizi.

Majina ya Asili ya Watoto Yaliyo na Maana Itokanayo na Misimu ya Miaka na Siku

Jamii ya Waasu huwapa watoto majina ya asili yaliyo na maana itokanayo na misimu ya miaka na siku. Majina hayo hutolewa kwa sababu watoto wamezaliwa katika vipindi hivyo ambavyo vinaweza kuwa masika, kipindi cha baridi, kipindi cha jua na hata kipindi cha njaa. *Jedwali 7* limefafanua.

Jedwali 7: Majina ya asili ya watoto yenye maana inayotokana na misimu ya miaka na siku

Jina	Jinsi	Maana	Jina	Jinsi	Maana
Kompeho	Ke	Baridi	Sekio	Me	Usiku
Mashika	Me	Masika	Sempeho	Me	Baridi
Nakio	Ke	Usiku	Semvua	Me	Mvua
Namvua	Ke	Mvua	Sevuri	Me	Vuli
Navuri	Ke	Vuli	Mpehongwa	Ke	Baridi

Misimu ya miaka ya siku ambayo wanajamii wa Kichasu wanapitia hutumika kuwapatia watoto majina ya asili. Wanajamii wanaamini na kuhusisha misimu au siku na ujio wa mtoto, hivyo inaweza kuwa siku yenye baraka au laana. Mfano mtoto anayezaliwa kipindi cha mvua hupewa jina la *Namvua* kama ni wa kiume, na *Semvua* kwa mtoto wa kike. Mtoto aliyezaliwa kipindi hiki anaaminika kuwa amekuja na baraka.

Majina ya Watoto yenye Maana Itokanayo na Majanga

Yapo majina katika jamii ya Waasu yanayotolewa kutokana na majanga yanayotokea katika jamii, mfano vita, njaa, ukame, mafuriko na magonjwa. Hivyo, watoto hupewa majina yanayosawiri majanga hayo. Rejea *Jedwali 8* hapo chini.

Jedwali 8: Majina ya asili ya watoto yenye maana itokanayo na majanga

Jina	Jinsi	Maana	Jina	Jinsi	Maana
Berya	Me	Mafuriko	Nanzano	Ke	Jua kali
Kazuva	Me	Jua	Navwasi	Ke	Shida
Matwatizo	Ke	Matatizo	Nkondo	Me	Vita
Mmasa	Me	Mgomvi	Nzota	Me	Njaa
Mshigwa	Me	Aliyeachwa	Senkondo	Me	Mtu wa vita
Nankondo	Me	Mtu wa vita			

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1826

Hivyo watoto waliozaliwa kipindi cha majanga mbalimbali hupewa majina hayo ili kutunza kumbukumbu ya matukio hayo kwa jamii husika.

Majina ya Asili ya Watoto yenye Maana Itokanayo na Vyakula

Yapo majina ya asili ya watoto yanayotokana na vyakula ambavyo ni vile vinavyotumika katika jamii ya Waasu; vyakula hivyo ni kama vile mahindi, mihogo, maboga, viazi vitamu, ndizi na maharagwe. Majina hayo yamefafanuliwa katika *Jedwali 9*.

Jedwali 9: Majina ya asili ya watoto yanayotokana na vyakula

Jina	Jinsi	Maana	Jina	Jinsi	Maana
Kapara	Me	Parachi	Naishwee	Ke	Ndizi iliyokataa kukomaa
Kashanga	Me	Boga bichi	Nakijo	Ke	Chakula
Kaunga	Me	Unga	Namawa	Me	Pombe
Kiogwe	Me	Kiazi	Nampunga	Ke	Mpunga
Kishumba	Me	Mtoli	Nampure	Ke	Kande
Makoko	Me	Maboga	Nandizi	Ke	Ndizi
Mmange	Me	Mhogo	Seivunja	Me	Mhogo uliovunda

Majina wanayopewa watoto yenye maana ya vyakula kama data inavyonyesha katika *Jedwali 9*, yanatolewa kwa sababu mzazi anapenda, au anafanya biashara au anakula vyakula hivyo kama vile maboga, viazi vitamu, mihogo, mahindi, ndizi na hata vinywaji. Hivyo, vyakula na mazao yanayopatikana na kutumika katika jamii ya Waasu hutumiwa kama majina ya asili kwa watoto kwa sababu ni vitu vilivyopo katika mazingira ya jamii hiyo.

Majina ya Asili ya Watoto Yenye Maana Itokanayo na Matukio ya Furaha

Jamii ya Waasu hupenda kuwapa watoto wao majina ya asili yatokanayo na matukio ya furaha. Hii ni kawaida kwa jamii nyingi kuhudhuria au kuandaa matukio ya sherehe kama vile harusi, jando na unyago na sherehe za siku ya kuzaliwa. Majina yanayohusu matukio ya furaha hutolewa kwa watoto wa kike na wa kiume kama inavyoonyeshwa katika *Jedwali 10*.

Jedwali 10: majina ya asili ya watoto yanayotokana na matukio ya furaha

Jina	Jinsi	Maana	Jina	Jinsi	Maana
Namseka	Ke	Nimecheka	Nimzihirwa	Me	Namfurahia
Namwai	Ke	Mwali	Tuzihirwe	Me	Tumefurahia
Nangasu	Ke	Unyago	Twamzihirwa	Me	Tumemfurahia
Nazahedi	Ke	Nimekuja pazuri	Twazihirwa	Me	Tumefurahia
Nazihirwa	Ke	Nimefurahi	Zihirwani	Me	Furahieni
Ngasu	Me	Sherehe yaunyago			

Katika jamii ya Waasu zipo sherehe mbalimbali za kijamii zinazofanyika za furaha au huzuni. Sherehe hizo hupelekea wanajamii kuwa na majina yanayoakisi matukio hayo. Hivyo watoto wanapozaliwa hupewa majina yanayohusiana na sherehe hizo mfano *Namwai* likimaanisha mwali, hili limetokana na sherehe ya harusi ambayo mwali huolewa na kuwafanya wanajamii kufurahia tukio hilo.

MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI

Sehemu hii inahusu mjadala wa matokeo ya utafiti kuhusu maana za majina ya asili ya watoto katika jamii ya Waasu. Mjadala huu umejikita katika malengo mahususi mawili ambayo ni kubainisha majina ya asili ya watoto na kuchambua maana zilizobebwa na majina ya asili ya watoto katika jamii ya Waasu.

Makala hii imeonyesha kuwa katika jamii ya Waasu yapo majina mengi ya asili wanayopewa watoto na yanaongezeka kila siku kwani watoto

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1826

wanazaliwa kila siku pia. Utaratibu wa utoaji wa majina katika jamii ya Waasu hutegemea ukoo husika. Zipo koo ambazo majina hutolewa na bibi au babu na kuna koo ambazo majina hutolewa na shangazi wa mtoto. Mfano katika ukoo wa *Wakwizu* majina ya watoto hutolewa na bibi mzaa baba pamoja na baba wa mtoto. Nadharia ya Uumbaji ya Sapir (1958) katika kusisitiza ubainishaji wa majina ya asili ya watoto, Sapir aliamini kuwa upo uhusiano wa lugha na jamii na pia lugha hutawala fikra za wazungumzaji wake na kuwapa namna ya kusawiri ulimwengu wao. Hata hivyo anasema ni vigumu kuchukua jina la jamii fulani na kumpa mtu wa jamii nyingine. Jina la jamii moja hufungamana na imani hiyo ambayo huambatana na utamaduni wa jamii husika. Vile vile Mbiti (1990) anasema katika imani za Kiafrika majina yana athari katika tabia ya mtoto, afya ya mtoto, mwenendo, mafanikio na hata maendeleo ya mtoto baadaye. Hivyo, kwa mujibu wa nadharia hii ubainishaji wa majina ya asili ya watoto katika jamii ya Waasu, unatoa mwanga kwa wanajamii kujua asili yao kwani majina hayo yanatunza utamaduni wao.

Matokeo yanaonyesha kuwa taratibu za utoaji wa majina hutegemea koo na koo kwani katika jamii ya Waasu zipo koo nyingi mfano *Mnkeni, Mkwizu, Mbwambo, Msuya* na zingine. Hivyo kila ukoo una utaratibu wake wa kutoa majina, wengine majina hutolewa na shangazi, wengine bibi au babu na wengine majina hutolewa na wazazi wenyewe wa mtoto. Matokeo yameonyesha kuwa yapo majina pia yanayorithiwa kutoka kwa bibi na babu waliopita katika familia husika.

Kwa ujumla majina ya asili ya watoto katika jamii ya Waasu ni mengi, baadhi ya majina hayo ni Nangasu, Mshigwa, Kireri, Namwai, Nyari, Nkondo, Nirindiwe, Namkunda, Mnavu, Mramba, Makoko, Najenjwa, Nkiru, Ndimangwa, Taseni, Lubwerere, Mweta, Nazahedi. Majina haya husaidia wanajamii kutunza kumbukumbu ya historia yao na utamaduni wao.

Aidha makala hii imeonyesha kuwa majina yote ya asili ya watoto katika jamii ya Waasu yana maana ambazo zinatokana na hali pamoja na vitu mbalimbali vilivyopo katika jamii ya Waasu. Majina hayo yamepangwa katika makundi ambapo matokeo yameonyesha kuwa yapo majina yenye maana itokanayo na imani kwa Mwenyezi Mungu, mahali au eneo mtoto alipozaliwa, wanyama, misimu ya miaka na siku, majanga, vyakula pamoja na matukio ya furaha.

Matokeo ya makala yamebainisha majina ya asili ya watoto yenye maana ya imani kwa Mwenyezi Mungu au dini ambayo baadhi yake ni *Gwirisha, Taseni, Nakombolwa, Nakijwa na Kazeni*. Masanja (2019) na Azael (2013) wanathibitisha kuwa yapo majina katika jamii ya wabantu ambayo hutolewa kwa sababu ya imani ya dini waliyokuwa nayo wazazi wa watoto. Suala hili limejitokeza pia katika makala hii kwa kuwa Kichasu pia ni mojawapo ya lugha za Kibantu. Kwa mfano jina *Taseni* lina maana ya kuomba kwa Mungu, jina hili hupewa mtoto ambaye wazazi wake ni watu wanaoomba sana kwa Mungu (wanamaombi). Katika jamii ya Waasu wapo watu wenye imani kwa Mungu au kwa miungu hivyo mazingira haya yanasababisha watoto kupewa majina hayo.

Makala hii pia imeonyesha kuwa yapo majina ya asili ya watoto yenye maana itokanayo na vyakula mfano *Kadio, Kiogwe, Kamange na Kashanga*. Leech (1974) anasema ipo maana ambayo huhusisha umbo, sifa na matendo ya kirejelewa. Jina *Kiogwe* katika Kichasu hupewa mtoto ambaye amezaliwa na wazazi wanaopenda viazi vitamu au wakulima wa viazi vitamu. Hivyo watoto wanaopewa majina yenye maana ya vyakula wanahusishwa na vyakula vinavyopatikana katika jamii yao. Hivyo kutokana na lugha ya Kichasu ambayo imetawala jamii hii na mazingira yake, huwapa watoto majina ya vitu ambavyo vipo katika mazingira yao. Pamoja na hayo, Rashidi (2017) anaonesha kuwa baadhi ya maana za majina zinapatikana kwa kuyahusisha majina hayo na shughuli au vitu fulani. Hivyo majina ya watoto wa jamii ya Waasu mengi yana maana zinazohusishwa vitu vilivyopo katika mazingira yao.

Halikadhalika, katika jamii ya Waasu yapo majina pia yanayohusishwa na majanga kama vile vita,

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1826

njaa na magonjwa, mfano *Senkondo, Berya, Nzota* na *Nanzano.* Mulokozi (1996) anafafanua kuwa watu katika makabila mbalimbali ya Kibantu hupewa majina ambayo maana zake zinahusianishwa na matukio mbalimbali kama kuzaliwa kabla ya wakati, njaa kubwa, na kuzuka kwa vita. Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kuwa jina *Nzota* anapewa mtoto aliyezaliwa kipindi cha janga la njaa, na jina la *Nanzano* hupewa mtoto aliyezaliwa kipindi cha jua kali linalosababisha ukame. Pia jina *Nkondo* linalomaanisha vita hupewa mtoto aliyezaliwa kipindi cha vita.

Aidha matokeo ya makala hii pia yanaonyesha kuwa yapo majina ya asili ya watoto yenye maana itokanayo na mahali mtoto alipozaliwa. Majina hayo ni *Nanzia, Sekiete, Mweta, Namshitu* na *Nakiete.* Katika jamii ya Waasu watoto hupewa majina ya maeneo walipozaliwa kwani wanaamini kuwa yana maudhui na umuhimu ndani yake. Mtoto anapoitwa *Namshitu* ikimaanisha wa msituni lina umuhimu kwake kwani linampa umaarufu fulani kuwa kama vile msitu ulivyojaa miti ndivyo naye atakavyokuwa na mafanikio mengi. *Mweta* ambalo ni mto tena mkubwa linampa mtu umashuhuri kuwa hakuna mtu atakayemshinda kama vile mto ulivyo na nguvu ndiyo mtu huyo atakavyo kuwa na nguvu.

Pia matokeo ya makala yameonyesha kuwa yapo majina ya asili ya watoto katika jamii ya Waasu yenye maana itokanayo na majira ya siku na miaka mfano *Navuri, Kompeho, Mashika, Nakio* na *Namvua.* Majina haya wanapewa watoto kwani jamii hii inapitia au inapata majira haya katika miaka na siku wanazoishi Waasu ikiwemo majira ya masika, majira ya vuli kipindi cha baridi na hata jua. Hivyo lugha ya Kichasu inaamua ulimwengu wao kuwa wawape majina gani watoto waliozaliwa katika majira hayo.

Aidha makala hii imedhihirisha kuwa yapo majina ya asili ya watoto yenye maana itokanayo na wanyama mfano *Nantembo, Sentembo, Naigonji, Nyaki, Fue* na *Kachua.* Kalekwa (2018) pia amebainisha majina ambayo maana zake zinahusishwa na mwonekano wa maumbile ya mtu katika lugha ya Kisukuma. Pia katika jamii ya Waasu yapo majina ya asili ya watoto ambayo maana yake inahusiana na mwonekano wa mtoto.

Kwa ujumla matokeo ya utafiti katika sehemu hii yameonyesha kuwa maana za majina ya asili ya watoto katika jamii ya Waasu yapo katika makundi ikewepo kundi la majina yenye maana itokanayo na imani kwa Mwenyezi Mungu, mahali au eneo mtoto alipozaliwa, wanyama, misimu ya miaka na siku, majanga, vyakula pamoja na matukio ya furaha.

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

Makala hii imechambua maana za majina ya asili ya watoto katika jamii ya Waasu. Malengo mahususi yakiwa kubaini majina ya asili ya watoto na kuchunguza maana zilizobebwa na majina ya asili ya watoto katika jamii ya Waasu. Matokeo ya utafiti yameonyesha kuwa katika jamii ya Waasu yapo majina ya asili ya watoto mengi ila katika makala hii watafiti wamebaini na kufanyia kazi majina 145. Baadhi ya majina hayo ni *Natogola, Nanzia, Kadio, Murindoko, Nietiwe, Nzota, Nainkwa, Gwagwala, Kireri, Mpoangwa, Mnavu na Kiogwe.* Makala imeonyesha kuwa majina ya asili ya watoto katika jamii ya Waasu yana maana zitokanazo na mazingira ya wanajamii. Yapo majina yenye maana itokanayo na imani kwa Mwenyezi Mungu, majanga, wanyama, misimu ya miaka na siku, majina yenye maana itokanayo na eneo mtoto alipozaliwa, vyakula na matukio ya furaha. Kutokana na matokeo haya inaonekana kuwa tafiti kuhusu majina katika jamii ya Waasu zimefanyika kwa kiasi kidogo hivyo tafiti zingine zinazofanana na utafiti huu zifanyike, aidha tafiti hizo pia zifanyike katika jamii zingine kwani jamii hutofautiana katika mila na utamaduni. Makala hii ina mchango mkubwa katika kuhifadhi historia, na utamaduni uliojificha katika lugha ya Kichasu. Matokeo ya makala hii ni sehemu ya utambulisho wa jamii ya Wachasu.

MAREJELEO

Agyekum, K. (2006). The Socialinguistics of Akan Personal Names. *International Journal*

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1826

of Humanities and Social Science, 15(2), 206–23.

Azael, R. (2013). Maana ya Majina ya Asili katika Jamii ya Kiuru.Tasnifu ya Umahiri katika Kiswahili (haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Baitan, B. (2010). A Mopho Semantic Analysis of Ruhaya Person Names. M.A. Dessertation (unpublished), University of Dar es Salaam.

Creswell, J. W. & Creswell, J. D. (2022). *Reseach Design: Qualitative,* Quantitative and Mixed Method Approaches. Califonia: Sage Publications. Inc.

Elihaki, Y. (2012). Majina ya Mahali katika Jamiilugha ya Chasu.Tasnifu ya Umahiri katika Kiswahili (haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es salaam.

Kalekwa, L. B. (2018). Uchambuzi wa Kiisimujamii wa Majina ya Koo za Kisukuma, Wilaya ya Misungwi. Tasnifu ya shahada ya Umahiri ya Kiswahili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Kihore, Y. M. (2009). *Isimu jamii Sekondari na Vyuo*. Chuo Kikuu Dar es Salam: TUKI.

Leech, G. N. (1974). *Semantics: The Study of Meaning*. Auxland: Penguin Books.

Lenjima, L. (2019). Kuchunguza Maana ya Majina Asilia ya Watu katika Jamii ya Wajita Mkoani Mara Nchini Tanzania. Tasnifu ya shahada ya Umahiri katika Kiswahili (haijachapishwa), Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Masanja, N. T. (2019). Uchunguzi wa Kisemantiki wa Majina ya Asili katika Koo za Ginantuzu. Tasnifu ya shahada ya Uzamivu ya Kiswahili (haijachapishwa), Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Massamba, D. P. B. (2009). *Kamusi ya Isimu na Falsafa*. Dar es Salaam: TUKI.

Mbiti, S. (1990). *African Religion and Philosophy*. USA: Heinemann Educational Books Inc.

Mulokozi, M. M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili.* Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Muzale, H. R. T. (1998). The Linguistic and Social Culture Aspects in Intercustrine Bantu Names. *Kiswahili, 2 (61), 28-29.*

Nyanganywa, M. (2013). Uchunguzi wa Kisemantiki na Taratibu za Utoaji wa Mjina ya Kijita. Tasnifu ya M.A Kiswahili (haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Nyiti, J. (2021). Maana ya Majina ya Koo katika Jamii ya Wameru: Tasnifu ya shahada ya Umahiri katika Kiswahili (haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira.

Ponera, S. A. (2019). *Misingi ya Utafiti wa Kitaamuli na Uandishi wa Tasnifu*. Dodoma: Central Tanganyika Press.

Rashidi, M. O. (2017). Michakato na Mbinu Zilizotumika katika Uundaji wa Majina ya Mitaa katika Wilaya ya Mjini Unguja. Tasnifu ya Shahada ya Umahiri katika Isimu ya Kiswahili (haijachapishwa), Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Resani, M. (2016*).* Maana katika Majina ya Wabena Nchini Tanzania. *Mulika, Na. 35.*

Resani, M. (2017). *Semantiki na Pragmantiki ya Kiswahili*. Dar es Salam: Karljamer Print Technology.

Sapir, E. (1958). *Language*. New York: Harcourt, Brace and Co.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.